**MAELEZO YA MKUU WA MKOA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE ALIYOYATOA KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO KUHUSU UTEKELEZAJI WA HOJA ZA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 20 JUNI, 2024.**

- ***Katibu Tawala wa Mkoa,***
- ***Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri,***
- ***Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,***
- ***Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kalambo,***
- ***Waheshimiwa Madiwani,***
- ***Kamati ya Usalama ya Wilaya,***
- ***Mkaguzi wa Mkuu wa Nje wa Mkoa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,***
- ***Wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Katibu Tawala wa Wilaya ya Kalambo,***
- ***Mkurugenzi Mtendaji,***
- ***Maafisa Tarafa,***
- ***Wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania………….**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Awali ya yote napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi sote kuwa na afya njema. Kwa namna ya pekee nimshukuru na kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa

weledi mkubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa. Namshukuru pia **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kutuletea fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wananchi kwenye Sekta za Afya, Elimu, Miundombinu ya Barabara, na Maji.

***Msheshimiwa Mwenyekiti,*** Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo katika kipindi cha miaka **mitano** imekuwa ikipata Hati Inayoridhisha. Niwapongeze sana kwa kuendelea kulinda hiyo hadhi kwa miaka mitano mfululizo.

***Msheshimiwa Mwenyekiti,*** Naomba sasa nizungumzie uchambuzi wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 hususani katika maeneo ya msisitizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kama ifuatavyo:

***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** Katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2022/2023 iliyotolewa April, 2024 ilionyesha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilikuwa na Hoja za miaka ya nyuma ambazo hazijafungwa **31** na Hoja za Mwaka huu (2022/23) ni **19** hivyo kufanya Jumla ya Hoja **50**. Pia Halmashauri ilikuwa na jumla ya maagizo sita (6) ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ambayo hayajatekelezwa hadi sasa. Natambua Katibu Tawala Mkoa kupitia barua na vikao mbalimbali amesisitiza juu ya kujibu Hoja hizi na kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kuepuka kuzalisha hoja zisizo za msingi. Kupitia Kikao hiki nimtake Mkurugenzi na Wataalam wake kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Nje kuhakiki Hoja hizi ili ziweze kufungwa. Na kuhakikisha kuwa **maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za mitaa (LAAC) yanatekelezwa ipasavyo**. Pamoja na Hoja hizi zipo Hoja ambazo ningependa kusisitiza hapa ambazo Halmashauri inatakiwa kuzifanyia kazi kwa haraka;

1. Kuhusu Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani, Mkaguzi amebainisha maeneo ambayo Halmashauri haifanyi vizuri katika Ukusanyaji wa mapato ikiwemo Mapato ya Kiasi cha **Shilingi 61,124,100.00** ambayo yamekusanywa lakini hayajawasilishwa

Benki, nikutake Mkurugenzi kuweka mikakati ya kuhakikisha Halmashauri inakusanya mapato kikamilifu lakini pia kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinawasilishwa Benki kwa wakati kama Sheria za Fedha zinavyoagiza. Natambua Katibu Tawala Mkoa kupitia Barua ya **tarehe 10 Juni, 2024** amekwishatoa maelekezo ya marufuku ya kutumia fedha mbichi na kuchukua Hatua Stahiki za kinidhamu na kisheria dhidi ya Watumishi waliotumia fedha mbichi na kufanya udanganyifu au hujuma ya mapato ya Halmashauri nami **nasisitiza ni marufuku kutumia fedha mbichi na wote waliohusika wachukuliwe hatua stahiki za kinidhamu na kisheria.** Vile vile katika ufuatiliaji uliofanywa na Mkoa umebaini kuwa yapo mapato katika Mfumo wa zamani LGRCIS yaliyokusanywa na Watendaji wa Halmashauri katika **kipindi cha mwaka 2022 hadi 2023 kiasi cha Shilingi 243,458,600** ambayo hayajawasilishwa benki hadi sasa. Nikuagize tena Mkurugenzi kuchukua Hatua Stahiki kuhakikisha Fedha hizo zinarejeshwa na Wahusika wanachukuliwa Hatua za kinidhamu na kisheria kwa kuzingatia Kanuni ya 36 - 37 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022.

2. Mkaguzi katika Taarifa yake amebaini kuwa Halmashauri imeshindwa kukusanya mapato katika baadhi ya vingufu ambavyo ilikasimia mfano Kodi ya Pango, Chanjo ya mifugo, Ushuru wa Madini, Ushuru wa Taka, Upimaji na Usajili wa Ardhi n.k. Hili limepelekea Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kufikia **asilimia 83%** tu ya makusanyo ambapo ilikusanya kiasi cha **Shilingi 1,689,549,489** kati ya kiasi cha **Shilingi 2,033,990,000.** Nimearifiwa pia kwa mwaka wa fedha 2023/24 mpaka jana tarehe 19 Juni, 2024 Halmashari ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,710,607,360.41** sawa na **asilimia 71%** ya kiasi cha **Shilingi 2,412,405,000.00** ambayo ilikasimiwa kwa Mwaka wa fedha 2023/24 ni Dhahiri kuwa Halmashauri haitafikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani. Nikuagize Mkurugenzi kuweka mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa

mapato na kuzuia mianya yote ya upotevu wa mapato na ubadhirifu wa makusanyo ya mapato ya ndani.

3. **Eneo la Ununuzi na Usimamizi wa Miradi,** katika taarifa ya CAG, imeonekana Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ina Udhaifu katika uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2011 kama ilivyorejewa mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 na 2016 pamoja na usimamizi wa Mikataba pamoja na Miradi. Eneo hili ndilo lenye Hoja nyingi kuliko maeneo mengine na limekuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa miradi, na kwa tathmini yangu mapungufu mengi katika miradi yanatokana na eneo hili la manunuzi hivyo Halmashauri inapaswa kutilia mkazo katika eneo hili la matumizi ya Mfumo wa Ununuzi na kukiimarisha Kitengo cha Ununuzi kuhakikisha kinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Ununuzi ili kuepusha Hoja. Baadhi ya Hoja katika eneo la Ununuzi na Miradi zilizobainishwa katika Taarifa ya CAG ni pamoja na: -

Kuwepo kwa Miradi ya Shule na Zahanati ambayo haijakamilika yenye thamani ya **Shilingi 237,500,000,** Mapungufu mbalimbali ambayo Mkaguzi ameyabaini katika ujenzi wa Jengo la Utawala ikiwemo kuchelewa kukamilika kwa mradi huu, Mradi kuanza kutumika kabla haujakabidhiwa, kuchelewa kumlipa Mkandarasi n.k., Maamuzi ya Bodi ya Zabuni kwenye Manunuzi ya kiasi cha **Shilingi 119,257,763** kufanywa na Wajumbe wachache, Kutokumika kwa nyaraka na hati msako za Zabuni zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwenye manunuzi yenye thamani ya **Shilingi 182,101,346,** Hati Msako za bei zilizotolewa kwa Wazabuni bila kuwa na maelezo ya bidhaa zilizonunuliwa kiasi cha **Shilingi 205,494,758,** Mapungufu katika taratibu za ununuzi na ujazaji wa nukuu za bei/hati msako za bei kutoka kwa wazabuni kiasi cha **Shilingi 97,208,382,** Mapungu mbalimbali katika ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi Shilingi **150,000,000.**

Ni dhahiri eneo hili linaitia dosari Halmashauri na kuendelea kufifisha juhudi za Serikali katika kukamilisha Miradi kwa thamani ya Fedha inayotolewa. Nimtake Mkurugenzi kuchukua hatua stahiki kurekebisha kasoro zote zilizojitokeza. Kuhakikisha Kitengo cha Manunuzi kinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria na Taratibu za Manunuzi na kuwachukulia hatua watumishi wote waliosababisha hoja hizi za manunuzi zenye viashiria vya uzembe, kutotimiza wajibu, na kutozingatia Sheria.

4. Serikali imeendelea kufanya maboresho ya Mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa kukusanyia mapato (TAUSI), Mfumo wa kusimamia mali za Serikali (GAMIS) pamoja na mifumo mingine ya fedha na utawala, Mkaguzi amebainisha mapungufu mbalimbali katika matumizi ya mifumo hiyo. Nikuagize Mkurugenzi kwa kushirikiana na Wataalam kuhakikisha kasoro zote zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinarekebishwa na mifumo hiyo inatumika kikamilifu.

   Pamoja na Matumizi ya mifumo Mkaguzi pia alibaini uwepo wa Mashine za Kukusanyia mapato (POS Mashine) nne (4) ambazo hazikuwa hewani kwa kipindi cha kuanzia siku 50 mpaka 204. Dosari hii inazorotesha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ili kufikia lengo lililokusudiwa. Nikuagize Mkurugenzi kufanya ufuatiliaji na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote waliosababisha.

5. Mkaguzi pia katika Taarifa yake amebainisha kuwepo kwa Gari la Halmashauri ambalo limezuiliwa na mtoa huduma kutokana na deni la **Shilingi 38,464,620, Natambua Katibu Tawala Mkoa** amekwisha toa maelekezo ya Halmashauri kuzingatia **na** kutekeleza **Waraka wa Hazina Na. 4 wa 2014/15, Waraka wa Hazina Na. 1 wa 2018/19 na Waraka wa Hazina Na. 1 wa 2023/24** ambayo inahusu ulipaji na uzuiaji wa madeni ya Serikali. Vilevile Mkaguzi amebaini kutengwa kwa kiasi kidogo cha kulipa madeni kiasi cha **shilingi 17,430,000.00** wakati inadaiwa kiasi cha **shilingi 2,665,287,000.00** madeni ya watumishi na kiasi cha **shilingi 366,991,000.00** madeni ya wazabuni.

Nikuagize Mkurugenzi kuhakikisha kuwa unaweka mkakati madhubuti na unaotekelezeka wa kulipa madeni yote ya wazabuni ili kupunguza na kuondoa malalamiko ambayo yanaharibu taswira ya Halmashauri na Serikali kwa Ujumla sambamba na kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya ulipaji wa madeni.

6. Mapungufu katika upelekaji wa asilimia 40 ya Mapato ya Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo ambapo CAG katika Taarifa yake amebaini kuwa Halmashauri ya Kalambo haikupeleka kiasi cha **Shilingi 210,286,826** cha Mapato ya Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo. Nikuagize Mkurugenzi kuhakikisha kuwa Matumizi yote yanayofanyika yanazingatia sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 na miongozo ya bajeti iliyowekwa na siyo vinginevyo.

   Vile vile Mkaguzi amebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilivuka na fedha za Miradi ya maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo bila kuzitumia, hii ni ishara ya udhaifu mkubwa katika utekelezaji wa Bajeti na uzingatiaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na miongozo yake. Nikuagize Mkurugenzi kuhakikisha kuwa Matumizi yote yanayofanyika yanazingatia sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 na miongozo ya bajeti iliyowekwa na siyo vinginevyo.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Pamoja na maelekezo niliyoyatoa wakati wa uchambuzi wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali naomba nitoe maelekezo ya jumla kwa Halmashauri yako ili kupunguza na kuepuka Hoja za Ukaguzi kama ifuatavyo: -

i. Nasisitiza hatua stahiki za kinidhamu na kiutumishi zichukuliwe kwa watumishi wote ambao wameonekana kusababisha hoja kutokana na uzembe bila kumuonea mtu kwa kufuata taratibu na Kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2022, taarifa hii iwasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kabla ya Tarehe 26 Juni, 2024.

ii. Kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Nje pindi wanapofanya Ukaguzi badala ya kusubiri Hoja za Ukaguzi na Wakuu wa Idara na Vitengo

husika wakatoe maelezo au ufafanuzi kwa wakaguzi badala ya kuwatumia Wasaidizi.

iii. Kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa ndani (Internal control systems),

iv. Halmashauri iimarishe usimamizi wa manunuzi kwa kuhakikisha Sheria na Taratibu za manunuzi zinafuatwa kikamilifu. Na kwa sasa Sheria mpya ya ununuzi wa umma ya mwaka 2023 na kanuni zake za mwaka 2024 zimeanza kutumika tarehe 17 Juni, 2024. Hivyo kwa miradi itakayotekelezwa kwa njia ya "Force account" hakikisheni kabla ya ununuzi kufanyika katika miradi ya maendeleo kuwepo kwa mchanganuo wa gharama (schedule of requirements/materials) ili kutoruhusu ununuzi holela wa vifaa au zaidi ya mahitaji.

v. Kuimarisha na kusimamia matumizi ya mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa manunuzi ya umma (NeST), Mfumo wa kukusanyia Mapato (TAUSI), Mifumo ya Malipo (MUSE na FFARS).

vi. Utekelezaji wa maelekezo haya pamoja na kuwasilisha mpango wa utekelezaji wa Hoja uwasilishwe Ofisini kwangu kabla ya tarehe 26 Juni 2024 ili taarifa hizi ziunganishwe na kutumwa TAMISEMI kabla ya tarehe 30 Juni 2024.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mwisho, Napenda kukushukuru tena wewe pamoja na Waheshimiwa Madiwani na timu ya Menejimenti ya Halmashauri kwa kunialika kuhudhuria kwenye kikao hiki muhimu. Aidha zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 Waheshimiwa Madiwani hamasisheni Wananchi kujitokeza kwa wingi ili mwakani watumie haki yao ya Kidemokrasia. Nawakumbusha pia kuwa mwaka huu 2024 kutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nawaomba tuwahamasishe wananchi kujitokeza kuchagua viongozi wao muda utakapo fika.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,
Mungu Bariki Halmashauri ya Kalambo.
Asanteni sana kwa Kunisikiliza.

Mhe. Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA RUKWA**